

SHIRIKA LA KUWEZESHA MAENDELEO

(ADP MBOZI)



Tupo kwa ajili ya kupambana na umaskini



Baadhi ya Viongozi na watumishi wa Shirika (2016)

Utangulizi

Shirika la ADP-Mbozi lilianza kama mradi mnamo mwaka 1986 na baadaye liliandikishwa rasmi kama mfuko wa udhamini tarehe 29 Novemba 1995. Hatimaye mwaka 2005 Shirika lilisajiliwa chini ya sheria ya mashirika yasiyo ya kiserikali Tanzania; sheria namba 24 ya mwaka

2002. Namba ya uandikishwaji ya Shirika ni 1639. Kwa muda wote wa utekelezaji Shirika limeendelea kupanuka kwa kuongeza maeneo ya kutoa huduma na pia kupanuka kwa aina ya huduma zitolewazo kulingana na mahitaji ya walengwa.

Dira ya Shirika

Jamii ya vijijini na mjini ina maisha mazuri yanayozingatia matumizi endelevu ya rasilmali

Utume wa Shirika

Shirika la ADP Mbozi linaongoza katika kuwezesha maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa watu wa hali ya chini wa vijijini na mjini Nyanda za juu kusini mwa Tanzania kupitia uendelezaji kilimo na lishe bora, ujasiriamali na masoko, kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabia nchi,, uhamasishaji wa jamii kwa masuala ya watoto, jinsia, UKIMWI na na utawala bora. Aidha shirika linaimarisha uwezo wake wa wa ndani ili kutekeleza vipaumbele tajwa hapo juu.

Amali za Shirika

- i) **Kujituma:** Tunaamini kujituma kwenye shughuli zetu kutaleta mabadiliko chanya kwenye Shirika letu na jamii tunayofanya nayo kazi.
- ii) **Kushirikishana:** Tunaamini kuwa maendeleo ya kweli yanaletwa kwa kushirikisha nguvu za wadau mbalimbali. Hivyo jamii tunayofanya nayo kazi ina mchango mkubwa sana katika maendeleo yao.
- iii) **Uwazi:** Tunajitoe kuwa wazi ndani ya Shirika letu na tutaambukiza tabia hiyo kwa jamii tunayofanya nayo kazi.
- iv) **Uaminifu:** Kujenga uaminifu miongoni mwa watumishi unatuwezesha kufanya kazi kama timu, na kuwezesha kufikia malengo yetu kwa haraka zaidi. Hivyo walengwa wa Shirika wakizingatia uaminifu wataweza kukamilisha malengo waliojiwekea kwa wepesi zaidi.

Muundo wa Shirika:

Chombo cha juu cha maamuzi ni mkutano mkuu ambao kwa kipindi hiki una wanachama watano waanzilishi na wanachama wanane wa kawaida. Mkutano mkuu umekasimu mamlaka ya usimamizi na udhibiti wa Shirika kwa Bodi ya Wakurugenzi. Mkurugenzi Mtendaji akisaidiana na Timu ya menejimenti anatekeleza shughuli za siku hadi siku za Shirika.

6. Maeneo ya kipaumbele ya Shirika

6.1 Uhakika wa chakula na lishe bora.

6.2 Ujasiriamali na uendelezaji masoko.

6.3 Kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabia nchi.

6.4 Kuhamasisha jamii kwa masuala ya (Watoto, Jinsia, VVU/UKIMWI na Utawala bora).

6.5 Uimarishaji wa Shirika.

7. Malengo mkakati na mikakati ya Shirika

7.1 Kuongeza uhakika wa chakula na kuboresha lishe

- Kuendeleza kilimo na mifugo endelevu
- Uhifadhi bora wa mazao
- Kuimarisha Bajeti ya chakula
- Uendelezaji wa matumizi ya lishe bora
- Matumizi ya teknolojia rahisi na sahihi



Kilimo cha mtama kwa maeneo yenye mvua haba

7.2 Kuimarisha ujasiriamali na upatikanaji wa masoko

- Kuimarisha vikundi vya wakulima
- Kuongeza elimu ya Biashara
- Kuimarisha upatikanaji wa taarifa za masoko.
- Kuhakikisha upatikanaji wa mitaji
- Kuimarisha ushirikiano kati ya wakulima na wafanyabiashara.



Kuunganisha wazalishaji na masoko

7.3 Kujenga mazingira rafiki na yenye afya kwa jamii.

- i. Kuimarisha usafi wa mazingira na upatikanaji wa maji safi na salama.
- ii. Kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

7.4 Kuongeza hamasa kwa jamii kwa masuala ya (Watoto, Jinsia, VVU/UKIMWI na Utawala bora);-

- Kuendeleza haki na usalama wa Watoto.
- Kuhamasisha usawa na usawia wa kijinsia
- Kuzuia maambukizi mpya ya VVU na kupunguza athari UKIMWI na WWKMH.
- Kuhamasisha utawala bora

7.5 Uwezo wa Shirika wa utawala na uongozi umeboreshwa ili kuimarisha uendeshaji;-

- Kuongeza uwezo wa fedha wa Shirika.
- Kuboresha sera, mifumo na taratibu.
- Kuboresha rasmali watu
- Kuboresha uwekaji wa kumbukumbu.
- Kuboresha utandaaji na ushirikiano.
- Kuendeleza utangazaji wa Shirika.



Kusaidia watoto wenye shida

Eneo la kazi

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo shirika litaendelea kutekeleza shughuli zake Nyanda za juu kusini mwa Tanzania.

Mbinu zinazotumika katika utekelezaji wa miradi;

Mbinu zinazotumiwa na Shirika ni;-

- 1.Kufanya kazi na walengwa kupitia vikundi
- 2.Kutumia wahudumu wa kujitolea
- 3.Kutumia myororo wa thamani
- 4.Kutumia mashamba darasa

- 5.Kuzingatia raslimali za asili ktika kilimo.
- 6.Kutandaa na kutumia wataalamu wa nje
- 7.Kushirikishana ujuzi ndani na nje ya Shirika.



Uendeshaji wa mafunzo vijijini

Kwa maelezo zaidi wasiliana na;-

Mkurugenzi Mtendaji,
Shirika la ADP Mbozi
Makao Makuu
S. L. P. 204, Mbozi, Songwe.
Simu. +255 (025)-2580095
& +255 0754 398342
Nukushi: +255 (025) 2580312
Barua pepe: info@adpmbozi.or.tz &
adpmbozi@yahoo.com
Tovuti: www.adpmbozi.or.tz

Tawi la Njombe
S. L. P. 40, Ilembula, Njombe.
0759 490037.

Tawi la Chunya
S. L. P. Makongolosi
Simu: +255 (0)767 072060.

Tawi la Songwe
S. L. P. Kanga
Simu: +255 (0)763 505 949.